

## **ATHARI ZA LUGHA ZA TOVUTI KATIKA MUSTAKABALI WA UFUNDISHAJI WA KISWAHILI**

Doris Jelimo

Chuo Kikuu cha Kenyatta  
doriakoech@gmail.com

na

Evelyn Mudhune

Chuo Kikuu cha Kenyatta  
everlinemudhune@yahoo.com.

### **Ikisiri**

Maendeleo ya Kiswahili awali yalidhihirika kupitia kwa nyanja za biashara, siasa, dini na baadaye elimu. Kwa sasa nchini Kenya elimu inachangia pakubwa katika ueneaji wa Kiswahili kwa kuwa Kiswahili kinafunzwa kama somo na ni lugha mojawapo kati ya lugha rasmi nchini Kenya. Hii ina maana ya kwamba takriban wanafunzi wote katika katika mfumo wa elimu Kenya wana ujuzi wa Kiswahili. Hii leo, jukwaa jipya la tovuti limeibua mitandao ya kijamii ambayo inatumika katika maenezi ya lugha ya Kiswahili. Mitandao ya kijamii hujumuisha matumizi ya lugha mtandao (*Netspeak*) inayotumia lugha andishi kielektroniki na ambayo huhusisha lugha kadha za kimaeneo. Nchini Kenya lugha maarufu ni Kiingereza, Kiswahili na lugha za kiasili. Mitandao hii imechangia katika kurahisisha mawasiliano kwa kwa sababu ya kuwa nafuu, hivi kwamba kiwango cha Kiswahili kinachotumika, na hasa kupitia kwa vifupisho huingiza athari hasi ambazo huenda zikaathiri mustakabali wa lugha ya Kiswahili. Makala hii itatumia nadharia ya Uvumbuzi wa Msambao, kuangalia baadhi ya sifa za lugha ya mtandao zinazobainika miongoni mwa watumiaji mbalimbali wa mitandao ya kijamii.